Jina..... Nambari ya mtahiniwa...../.....

Nambari ya Usajili.....

Jina la Shule.....

Mkondo wa Darasa.....

Tarehe.....

Sahihi.....

102/2
KISWAHILI
Karatasi ya 2
LUGHA
JUNI, 2013
MUDA: Saa 2 ½

102/ 2 Kiswhaili P2 – Lugha Jumanne 10.45 am – 1.15 pm

MUUNGANO WA BUNYORE – MARANDA (BUMA II)
MTIHANI TANGULIZI MWIGO, 2013
CHETI CHA KUHITIMU KISOMO CHA SEKONDARI (KENYA)

MAAGIZO

a) Andika jina lako, nambari ya usajili na mkondo wako katika nafasi ulizoachiwa.
b) Jibu maswali yote
c) Andika majibu yako katika nafasi ulizoachiwa katika karatasi ya maswali.
d) Karatasi hii ina kurasa 10 zilizopigwa chapa
e) Mtahiniwa ni lazima ahakikishe kuwa kurasa zote zimepigwa chapa sawasawa na maswali yote yamo.

Kwa matumizi ya mtahini pekee.

Swali	Upeo	Alama
1	15	
2	15	
3	40	
4	10	
	Jumla	

1. UFAHAMU (ALAMA 15)

Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali.

Takwimu za tafiti za umaskini kila mara huonyesha kuwa bara la Afrika ndilo bara maskini kabisa kote duniani. Takriban wakaazi kiasi cha asilimia themanini hawawezi kumudu kutumia dila moja kwa siku. Toka kaskazini hadi kusini, mashariki hadi magharibi mwa bara, makaazi ya mabanda yametamalaki. Wakaazi wengi hulala njaa kutokana na ukosefu wa chakula. Watu wa mitaani waliovaa mararuraru wamejaa katika mji ya bara hili. Swali ni: Je, kwa nini umaskini umeliganda bara la Afrika hivi mithili ya kupe? Kwa nini bara hili husalia katika lindi la uchochole?

Ili kuelewa sababu za umaskini kuganda barani Afrika, yampasa mtu ima fa ima kurejelea historia ya bara hili. Kwa kipindi cha karne nyingi, Afrika ilidhibitwa na walowezi pamoja na mabeberu. Wana wake ambao wangelistawisha bara kiuchumi walitwaliwa kimabavu na kupelekwa ughaibuni, huko wamefungwa minyororo, kustawish uchumi wa mabara mengine. Afrika ikaporwa nguvu ambayo ni rasilimali kuu katika ustawishaji wa uchumi. La kusistiza ni kuwa Afrika haikufidiwa kutokana na wizi huu. Badala yake iliongezewa mizigo mingine.

Baada ya kipinid cha biashara ya utumwa kumalizika, Afrika ilijipata katika janga jingine. Wakoloni wakallingili bara kwa pupa. Wakaligawanya katika koloni mbalimbali miongoni mwao. Wakaingiwa na wendawazimu kuiba malighafi ya bara hili. Wakaiba mashamba, madini, miti na cha maana walichokipata. Badala ya malighafi haya kutumika kunawirisha bara la Afrika, yaliimarisha uchumi wa walikotoka wakoloni. Afrika ikaachwa kuzidi kudidimia katika lindi la umaskini.

Wakiloni walipotoka barani Afrika na kuzipa dola nyingi za Afrika 'uhuru' waliacha mkururo wa madhila. Madhila haya hayangeikubalia Afrika kujikomboa kutoka katika biwi la uchochole. Tatizo la kwanza na kubwa zaidi ni wakoloni kugawanya na kukatakata Afrika katika mataifa mengi. Mgawanyo huu ukawa haukufuata utaratibu wowote. Kwa sababu hii, watu wa nasaba moja wakawekwa katika nchi tofauti.

Halikadhalika, mkoloni hakufanya juhudi zozote za kuanzisha viwanda ambavyo vingenyanyua uchumi wa Afrika na kuwatoa Waafrika katika biwi la ufukara. Palipokuwa na ari yoyote ya kuanzisha kiwanda, kilipoanzishwa hakikusaidia Afrika kiuchumi. Vilikuwa viwanda vya kupunguza zigo la bidhaa na kuzifanya kuwa nyepesi ili zisafirishwe kwa ajili ya viwanda vya nchi walizotoka wakoloni.

Kwa kipindi cha muda ambao mkiloni amekuwa na maingiliano na wakaazi wa Afrika, amehakikisha kuwa Mwafrika amekuwa mtegemezi wake. Malighafi ya Afrika yalipelekwa kutayarishiwa viwanda vya wakiloni. Kisha Mwafrika alirudishiwa zikiwa bidhaa kamili za kutumiwa. Mwafrika akaonyshwa kuwa chochote kilichotoka kwa wakoloni ni bora zaidi ya chake alichozalisha. Hii ikawa ni mbinu moja ya wakiloni kuwafukarisha Waafrika. Hata sasa, kilichotoka Ulaya, hata kama ni cha hali ya chini, huonekana bora zaidi kuliko alichozalisha Mwafrika.

Sasa hivi pana haja ya wana wa Afrika kufanya vikao vya dharura ili kujadiliana kuhusu suluhisho la tatizo hili sugu la umaskini barani. Lazima wawahimize Waafrika wote kudhibitiwe na Waafrika wenyewe. Wawahimize kuacha hulka za kukimbilia mataifa yaliyowafanya watumwa na kuwakalia kikoloni kwa misaada ya maendeleo. Misaada hii si ya dhati bali ni ya chati na hailengi kuondoa umaskini barani bali kuuendelza.

Pana jaha pia Waafrika kuwa na miungano ya kiuchumi. Miungano hii husaidia katika uteteaji wa soko pamoja na bei za bidhaa zao ikilinganishwa na taif amoja kuyaendeleza mambo haya. Halikadhalika, Waafrika wanapswa kutambua kile wanachotaka na kupanga mikakati ya kufikia mahitaji ya kimsingi kwa wananchi wake. Kwa mfano, uimarishaji wa miundo mbinu ambayo itachangia kuimarisha uchumi wa mataifa wahitaji kuwa mstari wa mbele badala ya ununuzi wa magari na ndege za hadhi za kuwabebea.

Maswali

a. Kutamalaki kwa umaskini barani Afrika kunadhihirishwa na nani? (alama 2)

.....
.....
.....

b. Onyesha sababu:

i. tatu zinazotokana na wakoloni na zimeendeleza umaskini barani Afrika. (alama 3)

.....
.....
.....
.....
.....
.....

ii. Mbili zinazotokana na Waafrika wenyewe zinazochangia umaskini wa bara la Afrika. (alama 2)

.....
.....
.....
.....

c. Umaskini barani Afrika unaweza kukabiliwa vipi? (alama 4)

.....
.....
.....
.....
.....
.....

d. Kwa nini neon 'uhuru' likawekwa katika alama za unukuzi? (alama 1)

.....
.....
.....
.....

e. Eleza msamiati ufuatao kama ulivyotumika katika taarifa. (alama 3)

i. Wangelistawisha.....

ii. Malighafi.....

iii. Kuwafukarisha.....

2. UFUPISHO (ALAMA 15)\

Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali.

Mabadiliko ya katiba yaliyofanywa katika kipindi cha kati ya mwaka 1964 na 1988 nchini Kenya yalisababisha kuwepo kwa serikali ya mabavu na isiyoruhusu maoni yaliyotofautiana na uongozi wa taifa. Mfumo wa utawala ulitoa mwanya fmyu sana kwa upinzani. Kipindi kati ya mwaka 1975 na 1988 kilishuhudia kuchukuliwa kwa hatua kali dhidi ya wapinzani wa serikali na uongozi ulitumia sheria ya uhalifu kuzuia fursa za kuikosoa hata ikikiuka maslahi ya wananchi. Upinzani uliitwa usaliti na sheria ya uchochezi ilitumiwa ili kuweka watu kizuizini bila ya kufikishwa mahakamani. Palibuniwa utaratibu wa kupanga foleni nyuma ya mgombea wakati wa kupiga kura mnamo 1988. utaratibu huu ulizua hasira nyingi miongoni mwa wananchi na wansiasa walioonewa uchaguzini.

Upinzani ulishika kasi sana mnamo mwaka 1989 na wananchi walitaka haki za binadamu ziheshimiwe na serikali iwekewe mipaka katika uongozi wake. Wananchi walihisi kuwa ilikuwa imekithiri katika kunyanyasa na kudhulumu wananchi. Hamasa hizi zilitokana na nchini na pia shinikizo za kutoka nje. Kwa hakika, ulikuwa wakati mwafaka na bora wa kuleta mabadiliko.

Kuporomoka kwa ukuta wa Berlin na kuanzisha mapinduzi ya kisiasa dhidi ya Ukomunisti katika zile nchi zilizoitwa Ulaya ya Mashariki na Umoja wa Kisovieti iliyozitawala serikali za nchi za Kikomunisti siku za nyuma sasa haikuwa na nafasi tena barani Afrika. Wanasiasa, watetwzi wa haki za binadamu hasa viongozi wa kidini, wanasheria na wakereketwa wa vyama huru vya wananchi kwa pamoja walitumia wasaa huo kuichagiza serikali ya Kenya kukifuta kifungu cha 2A cha katiba. Juhudi hizo hazikuwa na mafanikio siku za mwanzo. Serikali iliwaandama watetwzi na wahubiri wa mfumo wa vyama vingi vya siasa na ikawatia ndani.

Shinikizo la kundi la wafadhili wan chi za magharibi waliojiita 'Klabu ya Paris' lilisukuma bele gurudumu la mabadiliko. Masaada ya kiuchumi iliyokuwa ipewe nchi ya Kenya iliambatanishwa na sharti la kuitaka serikali ikubali mfumo wa vyama vingi vya

siasa na kuheshimu haki za binadamu. Misaada ya maendeleo ilisitishwa na Kenya ikawekwa katika kipindi cha majaribio ili ionyeshe jinsi inavyoyatekeleza masharti haya. Haya, pamoja na matatizo ya mipango ya kurekebisha uchumi ya Shirika la fedha la Dunia na Benki ya Dunia na upinzani wa ndani ya nchi, uliilazimisha serikali kubadili mawazo.

Maswali

a) Fupisha mambo muhimu katika aya ya kwanza kwa maneno baina ya 40 – 45.
(alama 9, utiririko 2)

Matayarisho

.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....

Jibu

.....
.....
.....
.....
.....
.....

b) Kaw kuzingaita yaa tatu za mwisho tumia maneno baina ya 40-45 kundodoa mambo yaliyochangia kuleta mabadiliko ya kidemokrasia nchini Kenya.
(alama 6, utiririko 1)

Matayarisho

.....
.....
.....
.....
.....
.....

Jibu

.....
.....
.....
.....
.....
.....

3. MATUMIZI YA LUGHA (ALAMA 40)

a) Eleza sifa mbili bainifu za konsonanti /h/ (alama 2)

.....

.....

b) Ukitolea mfano, eleza maana ya silabi wazi. (alama 2)

.....

c) Sahihisha (alama 1)
sikupenda vyenye aliuhairisha mkutano ule.

.....

d) Huku ukitoa mifano, tofautisha baina ya nomino za kipekee na nomino dhahania. (alama 4)

.....

.....

.....

.....

.....

e) Andika kwa udogo-wingi. (alama 2)

Rafiki yake mwanamme alimwua nyoka.

.....

f) Weka nomino shingo katika ngeli yake mwafaka. (alama 1)

.....

g) Akifisha: (alama 3)
baada ya kufanya mtihani wa kcse waziri mkuu alienda ngambo kwa masomo ya ziada kabla ya kujitosa katika siasa katika kampeni zake alizoea kusema ndo tunaweza hii leo anazindua kitabu cha tawasifu yake msingi wa siasa za Kenya.

.....

.....

.....

.....

h) Onyesha uamilifu wa viambishi katika neno (alama 2)

.....

.....

.....

.....

(i) Andika kinyume: (alama 2).

Audi yake anameza chakula kwa pupa.

.....

.....

(j) Tunga sentensi ukitumia aina zifuatazo za viunganishi: (alama 2)

i. Kiunganishi cha wakati

.....

.....

ii. Kiunganishi tegemezi

.....

.....

(k) Huku ukitoa mifano, taja miundo yoyote mitatu ya kiima. (alama 3)

.....

.....

.....

.....

(l) Ainisha vihisishis katika tungo ifuatayo. (alama 2)

Alhamudlillahi! Nimepata kazi! Wallahi ! Sitafanya ajizi!

.....

.....

.....

(m) Tambua na ueleze hali zinazojitokeza katika sentensi ulizopewa. (alama 2)

i) Ukichelewa hutanipata.

.....

ii) Kalale mtoto wewe!

.....

(n) Changanua kwa kutumia vishale. (alama 4)

Wachezaji walipewa zawadi nono kuwa walicheza vizuro sana.

.....

.....

.....

.....

.....

.....

(o) Tumia neon mzee kama: (alama 2)

i) Kivumishi.....

ii) Kielezi.....

(p) Unda nomino moja kutokana na neon takabari. (alama 1)

.....

(q) Taja na utolee mifano matumizi matatu ya neon vile. (alama 3)

.....

.....

.....

(r) Tambua maana mbili zinazojitokeza katika tungo ifuatayo. (alama 2)

Tesoti aliambiwa akomeshe uchokozi wake.

.....

.....

.....

.....

4. ISIMU JAMII (ALAMA 10)

a) Jadili aina tatu za makosa katika matumizi ya lugha. (alama 6)

.....

.....

.....

.....

.....

.....

b. Onyesha jinsi ya kukabiliana na makosa yanajitokeza katika matumizi ya lugha (alama 4)

.....

.....

.....

.....

.....

.....